



Mpango wa Ukaribishaji

Mpango wa Ukaribishaji wa Kent County: Ni mpango wa jumuiya unaonuiwa kushughulikia vipaumbele muhimu zaidi na vizuizi kwa Wamarekani Wapya katika Kent County ili kufanya juhudi ili kuhakikisha kuwa Kent County ni jumuiya inayojumuisha na kukaribisha zaidi. Maoni yalikusanywa kutoka kwa Wamarekani Wapya katika jumuiya yetu kupitia utafiti wa 800+ na vikundi lengwa 25. Data hii ilitumika kubuni Mpango wa Ukaribisha wa Kent County ambao uliundwa na jopokazi la zaidi ya mashirika 40 kote Kent County na kutolewa mnamo Septemba 2020.

Maoni kutoka kwa jumuiya yetu ya Wamarekani Wapya yalifichua vipaumbele hivi vitano kuu:

1. Uhuru wa kufanya kazi katika taaluma ninayopendelea
2. Uhuru wa kudumisha utamaduni, dini na mila zangu
3. Kufikia kiwango cha Kiingereza kinachotakikana
4. Kushiriki kikamilifu katika elimu, usalama na maisha ya siku zijazo ya watoto wangu
5. Wamarekani kuelewa utamaduni, dini, na hali ya maisha yangu

Mpango wa Ukaribishaji wa Kent County (KCWP) umepangwa katika kategoria tano:

1. Kushirikisha Jumuiya Zote
2. Kutumia kikamilifu Uwezo wa Kiuchumi wa Wamarekani Wapya
3. Kuboresha Ujuzi wa Wamarekani Wapya
4. Kuhakikisha Upatikanaji wa Huduma kwa Wote
5. Kuhakikisha kuwa Wakaazi wote wa Kent County Wako na Wanahisi Salama.

Husika

Kamati ya Uongozi ya KCWP, pamoja na jopokazi la mashirika zaidi ya 40 lilibuni malengo na vipimo kwa kila kategoria ili kuanza awamu ya utekelezaji wa KCWP. Ukaribishaji ni juhudi ya kimsingi kabisa na ni lazima iungwe mkono na hatua mbalimbali za jumuiya ili kuonyesha kwamba tunakaribisha Wamarekani wapya na tunajitahidi kuunda jumuiya ya ujumuishaji, kukubalika na mahali ambapo watu binafsi na familia zao watastawi. Hatua yetu inayofuata ni kubuni Muungano wa Mpango wa Ukaribishaji wa Kent, kikundi chenye mashirika mengi ili kujumuisha wanachama wanaoakisi jumuiya mbalimbali tunazohudumia. Wanachama wa Muungano wa KCWP watachagua kikundi maalum kilichopewa kipaumbele ambapo mtazamo na uzoefu wao wa kipekee utakuwa na matokeo zaidi. Ili kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Muungano wa KCWP wanajumuia wanaalikwa kukamilisha utafiti huu mfupi:



Maelezo ya Kimsingi

Kent County ni nyumbani kwa wakaazi kutoka takriban nchi 112 wanaozungumza zaidi ya lugha 40. Mpango wa Ukaribishaji wa Kent County ulianzishwa ili kuwakaribisha Wamerikani wapya na kuhakikisha kuwa wanahisi kukubalika ili tuweze kukua na kustawi pamoja. Katika mwaka wa 2018 na 2019 jumuiya yetu ilipokea tuzo za ruzuku ya Gateways for Growth. Gateways for Growth (G4G) ni mpango wa kitaifa ambao husaidia jumuiya kutengeneza ripoti zilizobinafsishwa za athari za kiuchumi kwa Mamerikani Wapya pamoja na usaidizi wa kupanga mikakati ili kubuni mipango ya sekta nyingi ili kuwa ya kukaribisha zaid na kujumuisha Wamarekani Wapya. Ni ushirikiano wa mashirika mawili, [Welcoming America](#) na [Baraza la Uhamiaji la Marekani](#) (lililotambulika hapo awali kama Uchumi Mpya wa Marekani). Grand Rapids ni mojawapo ya maeneo 71 tofauti katika majimbo 35 ambayo yamepokea usaidizi wa G4G. Kama mpokeaji wa ruzuku jumuiya yetu ilipata usaidizi wa kutengeneza ripoti ya utafiti wa kiuchumi iliyobinafsishwa kuhusu jumuiya yetu ya wahamiaji, na baadaye tulipewa usaidizi ili kutayarisha Mpango wa Ukaribishaji wa Jumuiya.

Data

Hapa kuna mambo machache muhimu kutoka kwa data iliyokusanywa:

- Wahamiaji walichangia 24.1% ya ukuaji wa idadi ya watu katika Kent County kati ya 2011 na 2016.
- Wahamiaji walichangia dola bilioni 3.3 kwa Mapato la Kent County. Familia za wahamiaji zilipata dola bilioni 1.3 katika mapato na zilikuwa na uwezo wa kifedha wa karibu dola milioni 950 (2016)
- Katika Kent County 27% ya wahamiaji walio na umri wa miaka 25 na zaidi na 21.8% ya wakimbizi walio na umri wa miaka 25 na zaidi walikuwa na shahada ya kwanza au zaidi (2016)
- Kulikuwa na wajasiriamali wahamiaji 2,031 katika Kent County (2019)
- Kulikuwa na wahamiaji 55,595 ambao nyumbani kwao ilikuwa Kent County ambao walichangia asilimia 8.6 ya watu wa Kent County (2019)

Viungo Muhimu:

Soma mpango kamili kwa Kiingereza au Kihispania hapa:

www.kentcountynewamericans.org

Pata maelezo ya hivi punde kupitia mtandao wetu wa kijamii:

www.facebook.com/KentCountyWelcomePlan

Mratibu wa Mpango wa Ukaribishaji:

Hollin De La Cruz: hollin.delacruz@kentcountymi.gov